

Maswali na Majibu

1. Mbona Sulemani alienda Gibeoni?
Kuwa na karamu ya shukurani na kutolea Mungu dhabihu.
2. Mungu aliambia Sulemani nini kwa ndoto?
Kwamba Mungu atampa chochote atakachochagua
3. Sulemani alichagua nini?
Hekima ya kutawala watu wa Mungu kwa hekima.
4. Sulemani alijenga nini? *Hekalu yenye watu wangeabudia Mungu.*
5. Hekalu ilijengwa wapi? *Yerusalemu kwa Mlima wa Moria.*
6. Nini ilifanyika wakati Sanduku liliwekwa kwa Hekalu?
Wingu la utukufu wa Mungu lilin'gaa na kujaza hekalu.
7. Sulemani alikuwa tajiri namna gani?
Mungu alimbariki. Wafalme wengi walilipa kodi kwake. Wafanyi biashara wake walileta utajiri mwingi kutoka nchi za mbali.
8. Nani alikuja kuona utajiri wa Sulemani na kusikia hekima zake.
Malkia wa Sheba.
9. Mbona Sulemani alianza kuabudu miungu.
Alioa wake wageni wengi na wakamfunza juu ya miungu.
10. Mungu alisema nini itafanyika kwa sababu Sulemani aliaabudu miungu?
Mungu atatoa sehemu ya ufalme wa Sulemani kwa mtoto wake.

Mistari ya kukariri

2 Mambo ya Nyakati 6:18 Mithali 1:7 Yakobo 1:5 – 6

Mazungumzo

Soma maneno ya Sulemani kwa Mithali 2:9 – 11. Tunajifunza nini juu ya utajiri na wake wengi kwa Sulemani

Kuandika

Soma 1 Wafalme 3:16 – 28. Andika vile Sulemani alitumia hekima yake kusuluisha ugomvi katikati ya mama wawili.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 24 Sulemani – mfalme wa hekima

SOMA 1 Wafalme 3: 4 – 15; 1 Wafalme 10:1 – 13

SOMO

Sulemani alipokuwa mfalme alikuwa na umri wa miaka 20 labda. Ufalme ulikuwa mkubwa sana kwa sababu Daudi kwa usaidizi wa Mungu, alikuwa ameshinda mataifa mengi sana. Kabla Daudi hajakufa aliambia Sulemani akumbuke kumpende Mungu na amtii. Sulemani alitaka kumfurahisha Mungu kwa hivyo aliita watu wote kwa mkutano wa shukurani hapo Gibeoni. Maskani (hema iliyotumiwa na watu kuabudu Mungu) ilisimamishwa Gibeoni. Sulemani alitolea Mungu dhabihu elfu moja ya kuteketezwa juu ya madhabahu na akashukuru Mungu kwa kuwapa huo ufalme na kuwa na amani kutoka kwa maadui wao.

Mungu alifurahi sana kwa sababu Sulemani alimpenda. Usiku huo Mungu alikujia Sulemani kwa ndoto na kumuuliza achague chochote alichotaka. Sulemani alijua kwamba yeye ni kijana mdogo na hatakuwa na maarifa ya kutawala taifa kubwa la Israeli. Sulemani alijua Israeli ilikuwa taifa teule la Mungu kwa hivyo alitawala kwa niaba ya Mungu. Kwa sababu alikuwa mdogo, alitaka kuwa na hekima ya kuendesha watu wa Israeli kwa njia za Mungu. Alikumbuka vile Mungu alikuwa amesaidia Daudi kutawala kwa hekima. Kwa hivyo aliuliza Mungu ampe hekima ya kutawala watu wake.

Mungu alifurahi kwa sababu Sulemani aliomba hekima ya kutawala watu. Sulemani hakuuliza kitu chochote chake; hakuuliza mali au sifa au maisha marefu. Mungu alifurahia chaguo la Sulemani - kwa hivyo akaahidi kumpa hekima tena atampa mali, sifa na maisha marefu! Sulemani alifurahia sana hiyo ahadi ya baraka za Mungu.


Mungu alimfanya Sulemani kuwa mtu wa hekima kuliko watu wote duniani. Alijenga majengo mazuri. Alikuwa na meli nyingi za biashara iliyotelea Israeli utajiri mwingi kutoka ulimwenguni kote. Sulemani alisema methali 3,000 na kuandika nyimbo 1,005. Alijua historia ya asili sana na hekima yake ilijulikana ulimwengu mzima. Sulemani alitawala watu wa Israeli kwa hekima.

Sulemani alijenga Hekalu vile Mungu aliaahidi Daudi. Mungu alikuwa ameeleza Daudi vile hiyo Hekalu ingejengwa, kwa hivyo Sulemani alijenga vivyo hivyo. Ramani yake ilikuwa kama Maskani lakini hii ilikuwa kubwa kuliko. Ilikuwa jengo nzuri na ya kifahari. Daudi alikuwa amekusanya fedha, dhahabu na shaba ili Sulemani afanye Hekalu nzuri.

Hekalu ilijengwa Yerusalemu juu ya Mlima wa Moria. Hapa palikuwa ni mahali pa kipekee, huenda ikawa ni mahali penye Ibrahimu alitaka kumtolea Mungu Isaka kama dhabihu. Pia Daudi alikuwa amejenga madhabahu pale.

Sulemani alichimba mawe meupe ya kujengea Hekalu. Watu wa kukata hayo mawe, Sulemani alitumia watu wa ujuzi kutoka Tiro. Mfalme wao, Hiram alikuwa rafiki wa Daudi. Hiram aliwapa pia miti ya mierezi na mivunje ili wajengee.

Hiram alipea Sulemani fundi wa ujuzi wa kujenga. Mahali Patakatifu Sana, walitengeneza na kufunika hizo miti ya mierezi kwa dhahabu. Walitengeneza vinara kumi vya dhahabu na vitu vingine vizuri vya kutumiwa kwa kazi ya hekalu. Pia walitengeneza bakuli kubwa ya chuma, iliyosimamishwa nyuma ya n'gombe ndume ya chuma; ilijazwa kwa maji yaliyotumiwa na makuhani kunawa.



Hekalu ilijengwa kwa miaka saba. Ilikuwa jengo nzuri ya kifahari. Ilikuwa katikati ili Waisraeli watumie kuabudia. Hekalu ilipomalizika kujengwa, Sulemani aliandaa karamu kubwa na kutoa dhabihu ya wakfu kwa Mungu. Sanduku la Mungu lililetwa ndani ya Hekalu.

Sanduku lilipowekwa ndani ya Patakatifu sana, mwangaza wa Utukufu wa Mungu ulin'gaa na ukajaza Hekalu kwa wingu. Hii ilionyesha watu kwamba Mungu alifurahi. Uwepo wa Mungu ulikaa katikati ya makerubi iliyokuwa juu ya Sanduku. Sulemani alibariki watu na kuomba.

Mungu alibariki Sulemani vile alikuwa amebariki Daudi. Mungu alimwambia Sulemani kwamba ufalme wake utakuweko milele na mfalme kutoka kwa kabila ya Yuda atatawala kiti cha enzi cha Daudi. Lakini Mungu alihadharisha Sulemani kwamba kama wafalme watakaotawala baada yake wataabudu miungu na kuongoza watu kumwacha Mungu, hapo Waisraeli watachukuliwa mateka kutoka kwa nchi yao.



Wakati Sulemani alikuwa mfalme, Waisraeli walikuwa na nguvu sana hata na utajiri. Daudi alikuwa ameshinda maadui wa Israeli, kwa hivyo Sulemani alikuwa na amani wakati wa utawala wake. Daudi alikuwa ameshinda nchi nyingi kwa hivyo ufalme wa Sulemani ulikuwa mkubwa. Sulemani alifanya biashara na Misri, Siria na Tiro na wafanyi biashara wake walileta mali nyingi sana. Wafalme wote wenye Daudi alishinda walilipa kodi kwa Sulemani. Sulemani

alikuwa tajiri sana. Wafanyi biashara walioenda mbali waliambia watu juu ya hekima na utajiri wa Sulemani. Wafalme wengi walikuja kuona utajiri wa Sulemani na kusikiliza hekima zake.

Malkia wa Sheba alikuja kumtembelea Sulemani. Hakuamini hadithi yote aliyoisikia kwa watu juu ya Sulemani kama ilikuwa ya kweli. Malkia wa Sheba alikuja Yerusalemu. Alileta zawadi nyingi za dhahabu, mawe za thamani na karafuu. Malkia wa Sheba alishangaa kuona utajiri na kusikia hekima ya Sulemani. Sulemani alikuwa tajiri na hekima kuliko vile alivyokuwa ameambiwa! Sulemani aliweza kujibu maswali magumu yote yenye aliuliza. Malkia aliona Hekalu ya ajabu yenye Sulemani alijenga na akajifunza kuhusu Mungu. Sulemani alimpa Malkia wa Sheba zawadi nyingi za manufaa na akarudi akiwa na mshangao mwingi kwa yote aliyoyaona.

Sulemani alikuwa na wake 300 na masuria 700. Wake wa Sulemani wengi walikuwa wageni na waliabudu miungu. Hawa wake walitoka kwa mataifa zenye Mungu alisema wasiwe na urafiki nao. Sulemani alipenda wake wake na wakamfunza juu ya miungu yao. Sulemani alianza kuabudu hizi miungu na kuwatolea dhabihu. Mungu alikasirikia Sulemani. Mungu alimwambia, kwa sababu anaabudu miungu, Mungu atagawanyisha ufalme wake mara mbili mwanawe atakapokuwa mfalme na kutawala baada yake. Sulemani alitawala kwa maika 40. Halafu akafa na mwanawe Rehoboamu alikuwa mfalme baada yake.